

Habari kuusu kufukuzwa nyumbani

Kwa sababu za kutokulipa kodi ya nyumba

JUA HAKI ZAKO

Hapa chini ni habari kuhusu haki zako kama mpangaji.

Ikiwa mmiliki wa nyumba anakuambia:

- Lazima utoke nyumbani kwake; [AU](#)
- Mkataba wako wa kukodi nyumba hautafanywa upya na ni lazima uondoke kutoka nyumbani kwake; [AU](#)
- Lazima uondoke kwa sababu Gavana ameondoa makatazo yaliyokuwepo.

USIKUBALI KUONDOKA **HAKIMU PEKEE NDIYE ANAYEWEZA KUKUFUKUZA NYUMBANI.**

SHERIA YA IOWA INALAZIMISHA

M pangaji ambaye hakulipa kodi ya nyumba mapema lazima apate taarifa kutoka kwa mmiliki wa nyumba.

1. Taarifa lazima iwe kwa maandishi.
2. Taarifa inapashwa isisitize kwamba mkataba wa kukodi nyumba utasitishwa ikiwa kodi ya nyumba haitalipwa munano siku 3
3. Inapashwa utumiwe taarifa kwa njia stahiki.
4. Kipindi hiki cha siku 3 kinakupa "haki ya kurekebisha mambo" kwa njia ya kulipa kodi ya nyumba mnamo siku hizo tatu.
5. Kisheria, ukilipa jumla ya kodi ya nyumba katika siku hizo tatu, mmiliki wa nyumba hawawezi kukufukuza.

UKWELI MUHIMU

Ikiwa huwezi kulipa kodi ya nyumba munamo siku 3, sio lazima utoke nyumbani mara moja.

Lazima mmiliki wa nyumba aombe kwanza hatua ya kukufukuza kotini.

HAKIMU PEKEE NDIYE ANAYEWEZA KUKUFUKUZA NYUMBANI.

TAARIFA

IOWA LEGAL AID

Iowa Legal Aid hutoa msaada kwa wakaaji wa Iowa wenye kipato cha chini wanaokabiliana na tatizo la kufukuzwa nyumbani.

Kwa kuomba msaada kutoka kwa Iowa Legal Aid:

- Ita namba 800-532-1275
- Wakaaji wa Iowa wenye umri wa miaka 60 na zaidi, wataita 800-992-8161
- Tuma ombi lako mtandaoni kupitia tuvuti www.iowalegalaid.org

HOME INC.

HOME, Inc hutoa ushauri wa bure na wa siri kwa watu wanaokabiliana na hatua za kufukuzwa kutoka nyumba wanazokodi au kupoteza nyumba unayolipia rehani kuwa yako.

- Piga simu 515-243-1277
- Soma kitabu cha HOME, Inc

EMBARC's CRISIS HELPLINE & VIRTUAL ACCESS CENTER (KITUO CHA MSAADA WA EMBARC NA NJIA YA UFIKIAJI)

EMBARC hutoa huduma za moja kwa moja kwa wahamiaji na wakimbizi kupitia mitando kumi (10) ya simu zinazounga mkono zaidi ya lugha 24 tofauti.

- Burmese - 515.207.9442
- Chin Dialects - 515.216.0974
- French - 515.216.0654
- Karen - 515.216.0143
- Karen - 515.216.0712
- Kirundi - 515.207.9614
- Kunama - 515.216.0745
- Lingala - 515.216.4329
- Spanish - 515.344.3936
- Swahili - 515.216.0611